

Jumuiya ya Kimataifa ya Wahitimu wa Al-Azhar
Mradi wa Kupinga Mitazamo Mikali -
Mfululizo wa Kupinga Mitazamo Mikali (1)

Maana ya Uraia

Mtunzi

Prof. **Abdul-Fatah Abdul GhaniyAl-Awary**

Kimetolewa na

Prof. **Muhammad Abdul Fadhil Al-Qusy**
Mjumbe wa Baraza kuu la Ulamaa
Makamu Mwenyekiti wa Taasisi

Kimefasiriwa na

Ust. Muhammad Reda Abd-Alwahab
Ust. Ahmad Raafat Al-Sayed

Kimehakikiwa na
Ust. Fadhili Mansour

Kimepitiwa na
Prof. Mshiriki **Sameh Anwar Bayoumi**



Jumuiya ya Kimataifa ya Wahitimu wa Al-Azhar
Mradi wa Kupinga Mitazamo Mikali -
Mfululizo wa Kupinga Mitazamo Mikali (1)

Msimamizi Mkuu
Prof. **Muhammad Abdul Fadhil Al-Qusy**
Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Mradi
Usama Yasin
Mkurugenzi Mkuu wa Mradi
Hamdullah As-Safty

Namba ya usajili: 26639/2018
Namba ya Kimataifa: 978-977-85462-6-2

Tahadhari

Haki zote zimehifadhiwa na Jumuiya ya Kimataifa ya Wahitimu wa Al-Azhar Al-Sharif, hairuhusiwi kusambaza au kurudia kusambaza, au kutengeneza kitabu hiki au sehemu ya kitabu, au kukihifadhi kwenye vyombo vya uchapishaji pasi na kutangulia kuwepo makubaliano kwa maandishi na Jumuiya.

Jumuiya ya Kimataifa ya Wahitimu wa Al-Azhar
Mradi wa Kupinga Fikra za Misimamo Mikali
Chuo Kikuu cha Al-Azhar, Nasr City, Cairo, Arab Republic of Egypt
Namba ya Simu: +202 – 23868114
Fax: +202 23868116
Email: info@waag-azhar.org
Tovuti: www.waag-azhar.org



مشيخة الأزهر
مركز الأزهر للترجمة
Al-Azhar Center for Translation (ACT)

(اللغة السواحيلية)

مفهوم المواطنة

Kimefasiriwa kwa Kiswahili chini ya anwani:

Maana ya Uraia

Kimechapishwa na Kituo cha Al-Azhar cha Ufasiri (ACT)

☎ (+202) 23868005
✉ azharcenter4trans@gmail.com
Al-Azhar Conference Center (ACC) Building,
4 Ismail El-Qabbany St. off El-Tayaran St.,
Nasr City, Cairo, Arab Republic of Egypt.
http://www.azhar.eg/act

The book cover design is a portrait of Al-Azhar Mosque by the French Artist Émile Prisse d'Avennes (1807-1879).
Chapa ya kwanza: 1438 AH/2017CE
Namba ya usajili: 23174/2017

ISBN:

©No parts of this publication may be reproduced, stored in a retrieval system, or transmitted in any form or by any means, electronic, mechanical or otherwise, without the prior permission of the publishers

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu

Utangulizi

Kwa uandishi wa Prof. Muhammad Abdul Fadhil Al-Qusy

Mjumbe katika Baraza Kuu la Ulamaa la Al-Azhar Al-Sharif

Katika kitabu chake kinachozungumzia *Funguzi za Mji wa Makka* Sheikh Mkuu “Muhydin Ibn Araby” anaelezea kwamba Mwislamu wa kweli: haiwezekani kuwa hivyo pindi akili inaposimama kukuwa kwake kwa kutopanda na kuongezeka, ni lazima - katika mahusiano yake na ulimwengu pamoja na Muumba wa ulimwengu - katika “Upandaji wa kiroho” hupanda kutoka hali ya kiakili inayoshuka na kwenda katika hali nyengine inayopanda, kinyume na hivyo basi anakuwa ni rehani wa mgando wa akili na alama ya ukavu na kifo!!

Upandaji huu wa kiroho hupanua peo zisizo na mwisho za ubinadamu basi viumbe vyote - mbele ya ubinadamu huo - wanakuwa wenye uhai wanajifungamanisha kwa Muumba wake pasi na kuongea, na kusujudu pasi na kumsujudia kiumbe, wanaona uwepo kwa muono mzuri wenye upendo, roho na utulivu, kwa hali hiyo basi watamiliki sifa zote za ulimwengu kwa umbali wake wenye kuonekana na usioonekana.

Lau mtazamo huu wenye kuonekana utaungana na sura ya Uislamu katika zama zetu za hivi sasa - zama za vitu vya maada - juu yake na chini yake basi ungekuwa

na athari kubwa kwenye nafsi yenye kiu ya haki, usalama na uadilifu, na kuwa ni tiba ya magonjwa mengi ya zama hizi na malalamiko yake pamoja na kugusa njia ya uelewa na akili itakayoangazia kwenye kiza na utando mkubwa.

Lau mtazamo huu wenye kuonekana utachanganyika na sura ya Uislamu katika zama zetu hizi, basi usingewakuta Waislamu isipokuwa ni watu waliofunikwa na nyoyo za huruma vifuani mwao wakipeana mikono kwa uzuri wakiumia kwa maumivu ya watu wanyonge na wanakuwa juu ya watu wa chuki na kinyongo, wala hawaoni kwa wanadamu sehemu zote isipokuwa ni nyoyo zinazozunguka kwenye uzuri wa haki, uadilifu pamoja na kuwa na maadili ya juu pasi na kuendesha vitendo vya utumiaji nguvu vyenye kupelekea uuaji, wala kuona mtando wa chuki wala damu ikimwagwa au shingo zikikatwa.

Inaonekana kuwa mtazamo huu wa wazi - ambao unachanganyika na hisia za busara - kwa masikitiko makubwa - umegeuka katika zama zetu za hivi sasa kutoka kinyume na kuwa kinyume … basi wenyewe upo wapi kwenye hiyo fikra mbaya ambayo imejengwa na watu wake kuwa “Uislamu” kwa ujumla wake na ukubwa wake pamoja na huruma yake umekumbatia hali ya “kupenda madaraka” na kujihusisha na usimamizi wa mambo. Uislamu mbele ya watu hawa umekuwa ni wenye kujifunga kwenye “Michezo ya Siasa” ambapo unaendesha mazoezi na michezo na kuondoka peo zake na malengo yake makuu na upepo!

Upo wapi huo mtazamo wa wazi unaotambaa kwenye maadili yao yasiyo sawa ambayo yamesaidia kupasua

ulimwengu makundi mawili: Kundi la watu wa Imani, na kundi la ukafiri wa kijinga ambao hakuna budi ya kuuondoa na kumalizana nao, kisha watu wake wakaanzisha - kwa mtazamo wa mchezo wa kisiasa - uharibifu katika nchi na umwagaji damu na mipasuko, baada ya vijana kuja na vitendo vya uadui na chuki kisha wakawaacha wakiendesha vitendo vya matumizi ya nguvu na uharibifu: Wakiwa na utashi wa matamanio ya utawala na kustarehe kwenye viti vya madaraka pamoja na kujiunganisha kwenye makazi ya watawala, kama kwamba hakuna kilichobaki kwenye Uislamu wote - misingi na maadili - zaidi ya madaraka yanayonyemelewa na utawala wa kujiinua na mbio za madaraka zenye kudharau roho za watu na kuruhusu umwagaji damu!

Upo wapi huo mtazamo wa wazi unaotambaa kwa hao wanajikosha na "Usalafu" na wakidai wao ndio warithi wake kisha wanaufanya huo Usalafu kuwa ni sitara ya udanganyifu pale walipoveshwa ujinga wa kiakili, chuki na mtazamo wa upande mmoja mpaka wakazamisha mambo muhimu ya Waislamu katika mandhari za nje na mitazamo isiyo na afya ambayo imefungua mlango uliogemewa hapa baadaye wa madai ya ugaidi kila sehemu, ninakusudia kile walichokiita katika madili yaoyenye kuenea "Kulipiga kundi lenye kuzuia", lile wazo ambalo linakaribia kuwa shari ambayo imejikita kiimani kwa makundi mengi ya matumizi ya nguvu ya hapo zamani na hata ya sasa.

Upo wapi huo mtazamo wa wazi wenye kutembaa kwenye makundi haya ya kigaidi yenye majina ya kuchukiza ambayo yameitwa katika zama zetu hizi yenye

kulenga kusambaza uongo na uzushi kwa jina la Uislamu na ukhalifa wa Kiislamu, kisha walinganiaji wake kwenye nchi mbalimbali wanaendesha vitendo vya mauaji, kuchezea miili ya wafu, kukata shingo za watu mbele ya macho ya ulimwengu na kuona kwake kusiko pepesa jicho, au kugonga nyoyo zao pasi na kuangalia sifa zao kwa kukadiria kiwango cha uhalifu ambao wameufanya dhidi ya Uislamu pale wanapokutanisha sura ya Uislamu na sura ya damu pamoja na ukataji wa shingo za watu, bali pindi wanapoubadilisha Uislamu kwa athari za vitendo vyao hivi - katika mtazamo wa wengi - na kuwa ni “Ugonjwa” unaokumba ulimwengu wote, na inakuwaje sura ya ndani ya akili ambayo inajikita katika kumbukumbu za “Watoto Ulimwenguni” kuhusu “Uislamu” ambao wanadai kuinua bendera yake na kuinua neno lake!!

Kisha watu hawa na hao wengine hawageuki na kuangalia “*Jihadi ya Kiroho*” ya Kiislamu kwenye pande mbalimbali zinazopasa mwanadamu kuinua kwenye peo za juu kiroho, kiakili na kifikra kutako hamasisha ubinadamu kuimarisha kwa watu wake wenye njaa walio uchi na wagonjwa chakula, madawa, maisha bora na kumaliza ubinafsi mbaya ambao umezalishwa na ustaarabu wa manufaa.

Katika mfululizo huu wa kielimu tunajaribu kurudisha haki sehemu yake na kumaliza kile kilichogandishwa kwenye Uislamu na hao watu ikiwa ni pamoja na makosa mbalimbali ili tupate kuwaonesha vijana ukweli wa Uislamu na yanayopaswa kwao kuwa katika njia yao ya kuelekea kwenye kupata radhi za Mola wao na kumfuata Mtume wao S.A.W.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu kuafikisha haya na kukubali kwani Yeye ni mbora wa kuombwa na kwake ndiko kwenye matumaini makubwa.

Maana Sahihi ya Msamiati Uraia

Uraia: Inamaanisha mtu kupenda nchi yake na kuitetea.

Uraia ni: Kutendeana kati ya mwananchi na nchi ambayo anaishi na kujinasibihsa nayo, nao unahitaji kujinasibisha na mapenzi yake kwa nchi ambayo anajinasibisha nayo na kuitetea.

Mtu kupenda nchi yake ni mapenzi ya kimaumbile yanazaliwa na mwanadamu mwenye ufahamu salama, na wahenga wanasema "Kupenda nchi ni katika Imani" na pamesemwa tena: "Ukitaka kujua uaminifu wa mtu, basi angalia huruma yake kwa nchi yake".

Sharia za mbinguni zimekuja kusisitiza maana hii nzuri ya uraia, na zinahimiza kupenda nchi, kushikamana nayo na kuitetea, bali zimewajibisha Jihadi kwa ajili ya kutetea nchi, na zikamzingatia anayeuwawa katika kulitetea taifa lake na nchi yake kuwa anakufa shahidi.

Qurani Tukufu imesisitiza mtu kupenda nchi yake ikibainisha kuwa kuwafukuza watu nchini mwao ni sawasawa na kuua ambako kunamtoa mtu katika idadi ya walio hai. Mwenyezi Mungu Mtukufu Amesema: ﴿**Na lau kuwa Tumewaamrisha: Jiueni, au tokeni majumbani kwenu, wasingelifanya hayo ila wachache tu miongoni mwao. Na lau kama wangelifanya waliowaidhiwa ingelikuwa bora kwao na uthibitisho wa nguvu zaidi**﴾{An-Nisaa, 66}.

Miongoni mwa ahadi ambazo Mwenyezi Mungu Amezichukua kwa wana wa Israel ni zile ambazo zinasisitiza maana hii - kwa maana kuwatoa watu katika nchi zao na kuwazuia kuingia ni sawa na kumwaga damu

na kuwatoa katika maisha - Mwenyezi Mungu Mtukufu Amesema: ﴿**Na Tulipochukua agano lenu kuwa hamtamwaga damu zenu, wala hamtatoana majumbani mwenu; nanyi mkakubali nanyi mnashuhudia * Kisha nyinyi kwa nyinyi mnauwana, na mnawatoa baadhi yenu majumbani kwao, mkisaidiana kwa dhambi na uadui. Na wakikujieni mateka mnawakomboa, na hali kuwatoa mmekatazwa. Je! Mnaamini baadhi ya Kitabu na mnakataa baadhi yake? Basi hana malipo mwenye kutenda hayo miongoni mwenu ila udhalili katika maisha ya duniani, na Siku ya Kiyama watapelekwa kwenye adhabu kali kabisa. Na Mwenyezi Mungu si mwenye kusahau yale mnayoyatenda**﴾{Al-Baqarah, 84: 85}.

Na Mtume S.A.W. ametufundisha mtu kupenda nchi yake alipohamia Madina ambapo alibainisha mapenzi yake kwa Mji wake Mtukufu wa Makka, imepokewa Hadithi kutoka kwa Abdillah Ibn Addiy Ibn Hamraa R.A. amesema: Nimemuona Mtume S.A.W. akiwa amesimama eneo la Al-Hazura, akasema: "*Naapa kwa Mwenyezi Mungu hakika hii ni ardhi bora ya Mwenyezi Mungu, na ardhi Anayoipenda zaidi Mwenyezi Mungu katika ardhi zake, na lau kama wasingenitoa kwako nisingetoka*".

Na imepokewa Hadithi kutoka kwa Abdillah Ibn Abbas *Allah awawie radhi* amesema: Mtume S.A.W. aliiambia Makka: "*Uzuri wako ulioje, na unapendeza*

zaidi kwangu, na lau kama watu wangu wasingenitoa nisengekaa mji mwingine"[1].

Uhusiano huu kati ya mtu na nchi yake ikiwa ni pamoja na uzalendo, upendo na kuitetea kwake ni hisia iliyopatikana ndani ya zama zote na kwa raia wote, katika tamaduni za raia na jamii na fasihi zake kuna uwanja mpana ulioelezewa na hao raia na jamii juu ya upendo wao kwa nchi yao na miji yao, na kushikamana kwao na ardhi ambayo wamezaliwa na kulelewa humo. Kazi nyingi maarufu za kifasihi zinasifu watu kuwa na nia safi na nchi zao, kuwa tayari kufa kwa ajili ya kutetea uhuru wake na heshima yake. Nyimbo na nembo za taifa zimesaidia kuwaunganisha raia katika kutetea nchi zao nyakati za vita, na raia siku zote wanafanya kazi ya kudumisha roho ya uzalendo kwa kuheshimu kumbukumbu, matumaini na desturi, na kuwafundisha wanafunzi kupenda nchi zao na kuwaheshimu mashujaa wao na viongozi wakubwa wa taifa, mfano: Bendera ya taifa, sehemu za taifa za heshima na majengo ya kumbukumbu[2].

Waarabu walikuwa wakisafiri hubeba mchanga wa ardhi yao ili kunusa harufu yake na huutia kwenye maji pindi wanapokunywa[3].

Uraia unamaanisha usawa kati ya raia wote katika haki:

---

(1) Imepokelewa na At-Tirmidhy katika kitabu chake mlango wa *Ubora wa Mji wa Makka* ni Hadithi mbili 3925, 3926, na akasema kwenye Hadithi hizo mbili: Ni Hadithi Hasan Sahihi na Gharib.

(2) Kamusi elezi ya Kiarabu ya Kimataifa, mada, Uzalendo.

(3) Sherehe ya Kitabu cha Nahaj Al-Balagha, 1/91.

Na uraia unanasibishwa kwa raia wote ambao wanaishi katika nchi moja pasi na tofauti kati yao, unalazimisha usawa kati yao katika haki zinazotokana na kunasibishwa na nchi kwa kuzingatiwa kuwa ni asili zinaingia ndani yake haki za binadamu, kunapatikana marejeo ya kutekeleza Aya ambazo zimethibitisha kutokuwa na tofauti kati ya mtu na mwengine ndani ya taifa moja na nchi moja.

Mtume S.A.W. ametoa mfano wa ushirikiano wa kikamilifu na mahusiano yaliyopo kati ya wakazi wa nchi moja ni kama wasafiri walio kwenye meli moja yenye tabaka mbili, wakawa wale wa chini wakihitaji maji ya kunywa hupanda juu, wakasema baadhi yao: "*Lau tungetoboa katika tabaka letu kitobo ili tusiwasumbue walio juu yetu*", na akaelezea hilo Mtume S.A.W. kwa neno lake: "*Wakiwaacha wafanye walitakalo wataangamia wote, na wakiwazuia wataokoka na kuokoa wote*"[(1)].

Mtume S.A.W. baada ya kufika Madina akaweka katiba inayojenga mahusiano kati ya Waislamu wenyewe kwa wenyewe na Waislamu na wasiokuwa Waislamu, na katiba hii ilijulikana kama Waraka wa Madina, mpaka ukafikia upeo wa usawa katika haki za raia kiasi ambacho imeandikwa katika waraka huo ahadi ya Mtume S.A.W. kwa Wakristo kusaidiwa na dola ya Kiislamu watakapohitaji kujenga nyumba zao za ibada na kuzifanyia ukarabati, basi ikaja katika ahadi na Mkataba wa Mtume: "*Na wana haki wakihitaji msaada kukarabati Makanisa yao nyumba zao za Utawa au chochote katika*

(1) Imepokelewa na Imamu Bukhari katika Sahihi yake - mlango wa mambo ya ushirika, 3/139, nambari 2493.

masilahi ya mambo yao na Dini yao, na kuimarisha ukarabati wasaidiwe hilo, na wala lisiwe deni kwao, bali kuimarisha maislahi ya Dini yao na kutekeleza ahadi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu kwao na wema kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwao ...".

Hata katika masuala ya kifedha na kiuchumi kama vile kodi, yameandikwa katika Mkataba wa Mtume S.A.W. kwa Wakristo kwamba: "*Kutokemewa wala wasilipishwe isipokuwa kiwango wawezacho na nguvu yao ya kufanya kazi na kuimarisha ardhi na kupokea matunda yake, wala wasilazimishwe kwa nguvu wala watu wa kodi wasikiuke mipaka kwao viongozi wao ...*".

Haki zote za usawa katika uraia ambazo Uislamu umeziweka kwa wasiokuwa Waislamu katika nchi ya Kiislamu "Wao wana haki na wajibu walionao Waislamu" kulinda nafsi, damu, mali, heshima na sehemu za ibada na uhuru, kwa mkabala wa utiifu kamili kwa nchi na kujinasibisha moja kwa moja na jamii, dola na umma, nao ni wajibu wa raia wote Waislamu na wasiokuwa Waislamu.

Na katika kuthibitisha wajibu huu Mkataba wa Mtume S.A.W. umeandika: "*Na wameshurutishwa kwao mambo ambayo ni wajibu kwao katika Dini yao kushikamana na kutekeleza waliyoahidiwa, ikiwemo: Kutokuwa yeyote miongoni mwao jasusi wa adui wa Waislamu kwa siri na kwa wazi, wala wasiwakaribishe maadui wa Waislamu majumbani mwao, wala wasimsaidie adui yeyote wa Waislamu kwa silaha au farasi wala watu au vyenginevyo, wala wasiwasaidie na wasiwafiche kwa Waislamu, wala wasidhihirishe aibu zao kwa adui ...*".

Vilevile mkataba wa Mtume S.A.W. kwa Wakristo umeandika kuhusu uhuru wa kidini, kwani imekuja ndani yake: "*Wala asilazimishwe Mkristo yeyote kuingia kwenye Uislamu,* ﴿**Wala msijadiliane na Watu wa Kitabu ila kwa njia iliyo nzuri kabisa, isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao. Na semeni: Tumeyaamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu. Na Mungu wetu na Mungu wenu ni Mmoja. Na sisi ni wenye kusilimu kwake**﴾{Al-Ankabout, 46}. Na watazamwe kwa jicho la huruma, na wasifanyiwe maudhi popote walipo ndani ya miji yoyote ya Kiislamu ...".

Bali usawa huu kamili katika haki ya kiraia na wajibu wake wa kuwa wana haki na wajibu kama Waislamu wana wajibu waliokuwa nao Wakristo ili wawe washirika katika haki na wajibu, "Dola ya Kiislamu haikusimamisha hali hiyo kwa Wakristo na Mayahudi tu, bali ilikusanya na wafuasi wa dini za kutungwa miongoni mwa majusi na wengineo.

Ikiwa uraia na haki zake vimetambulika na nchi za Magharibi baada ya kuondoka mifumo ya dini, na baada ya mifumo ya usekula kulishinda Kanisa la Magharibi, kwa hiyo ndio ukaja uraia wa kisekula, bali Uislamu ndio umeanzisha uraia, na Sharia zake ndizo zimetambua haki zake na kudhamini kuzilinda ili isiwe “zawadi” kupewa na kiongozi na kunyimwa na mwengine"[(1)].

Misingi ya uraia

(1) Mjukumuiko wa nyaraka za kisiasa katika zama za Mtume S.A.W. na zama za Makhalifa waongofu, kitabu cha Dkt. Muhammad Hamidullah, uk. 75.

Hakika uraia una haki za msingi lazima zifikiwe ili kupata matunda yake yanayotarajiwa, miongoni mwa misinig hii ni:

1. Kushikamana na tabia za Kiislamu na kujiepusha na mabaya yake, kuchunga haki za binadamu na kuzitekeleza, kuanzia haki za wazazi wawili na ndugu mpaka haki za jirani na marafiki, na matumizi mazuri ya haki na maeneo ya umma, kila mwananchi kushughulika kwa dhati ili kulinda mali na nafsi za watu wengine.

2. Kutekeleza makubaliano na kuheshimu mikataba: Nalo ni jambo limehimizwa na Qurani na imebainisha kwamba hilo linatangulizwa katika kutetea Dini, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu Amesema: ﴿**Lakini wakiomba msaada kwenu katika Dini, basi ni juu yenu kuwasaidia, isipokuwa juu ya watu ambao yapo mapatano kati yenu na wao. Na Mwenyezi Mungu Anayaona mnayoyatenda**﴾{Al-Anfal, 72}.

3. Uadilifu kati ya raia: Nao ndio msingi na nguzo kubwa, ni jambo la kawaida kwamba msingi wa Sharia zote katika kushirikiana na watu wote ni uadilifu, hakuna kuacha hata kuwa na hali gani ya chuki kwa wengine, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu Amesema: ﴿**Wala kuwachukia watu kwa kuwa walikuzuilieni kufika Msikiti Mtakatifu kusikupelekeeni kuwafanyia uadui. Na saidianeni katika wema na ucha-Mungu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu**﴾{Al-Maidah, 2}.

Na Akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Enyi mlioamini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mkitoa ushahidi kwa haki. Wala**

kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na ucha-Mungu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Anazo habari za mnayoyatenda﴾{Al-Maidah, 8}.

4. Kuipenda nchi uliopo na watu wake ambao wewe ni miongoni mwao:

Na miongoni mwa misingi ya uraia vilevile: Kuipenda nchi ambayo wewe unaishi humo na watu ambao wewe ni miongoni mwao, hapana shaka kwamba kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kuwatii ni miongoni mwa misingi mikubwa ya Imani, lakini hili halimaanishi kuna ulazima wa kutopenda vyengine, huu ni mfano wa Mtume S.A.W. alipohama Makka baada ya mazingira ya Makka kukataa Uislamu na kuwatesa wafuasi wake, Mtume S.A.W. aliiangalia Makka akiiaga kwa huzuni na kusema: "*Ama naapa kwa Mwenyezi Mungu nakuacha na hakika mimi ninajua kwamba wewe ni mji niupendao zaidi miongoni mwa miji ya Mwenyezi Mungu na Mtukufu zaidi kwa Mwenyezi Mungu, na lau si kama watu wako kunifukuza nisingetoka*" **(1)**.

Na Masahaba wa Mtume S.A.W. walipopatwa na homa kali walipokuwa Madina Bilal R.A. alikuwa anaimba kwa sauti akisema:

Ehee shairi langu je, nitalala usiku mmoja -

---

(1) Imepokelewa na Abu Yaaly Al-Muuswily katika kitabu cha Abn Abbas RA 5/69, namba 2662 na akasema: Wapokezi wake ni watu sahihi ukiondoa Mahmuod Ibn Khaddash naye ni anaaminika.

katika bonde na pembezoni mwangu kuna mti wenye harufu nzuri

Na je nitakunywa siku moja maji laini - na je nitaona mimi milima ya Shama na Tafil[1].

Katika beti hizi mbili Bilal anawaza kumbukumbu za Makka mji wake ambao amelelewa na amekulia humo, na beti hizi zinatoa taswira ya mapenzi ya Bilal kwa nchi yake katika moyo wake, pamoja na kwamba ameuacha mji huu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake[2].

Mahitaji ya Uraia Mwema

Kumuelimisha raia umuhimu wa sehemu ya nchi yake, uwezo wake na historia yake, na mtu maarufu wa nchi hiyo, siasa yake ya nje ambayo inaheshimiwa na jamii ya kimataifa, na upekee wa jamii ambayo anaishi humo na mazuri yake, miongoni mwa hayo ni pamoja na: Ukati na kati, kuhurmiana, mapenzi na ushirikiano katika mambo mema na ucha - Mungu ili iwe sehemu ya kujifaharisha na kujipa nguvu.

Kupandikiza mapenzi ya nchi katika nafsi za raia na kuyaendeleza ili wazidi kujifaharisha na nchi yao, na kupupia kuinua taifa na kujenga hamasa ya kutetea

---

(1) Yamepokelewa na Imamu Bukhary katika sahihi yake – kitabu cha mambo ya mgonjwa – sura ya mwenye kutoa wito wa kuondoa jenga na homa 7/122 nambari 5677.

(2) Kitabu cha Misingi ya uraia ndani ya Qurani na Sunna pamoja na Sira za Mtume cha Sheikh Muhammad Zaaid Nadheer Ahmad, makamu rais wa Chuo Kikuu cha Kiislamu nchini Pakistan utafiti umechapishwa kwenye kitabu cha mambo ya ugaidi na hatari zake kwa amani ya dunia, ni mfululizo wa tafiti za Jopo la utafiti wa mambo ya Kiislamu uk. 131: 133.

heshima yake na ardhi yake, pamoja na kuendeleza kujifaharisha kujinasibisha na Umma wa Kiarabu na Kiislamu na kukinai umuhimu wa kushirikiana na mataifa ya nje.

Kuimarisha misingi ya Kiislamu na kijamii yenye sifa nzuri kwa wananchi, kama vile ushirikiano, ukweli, uaminifu na subira.

Kubainisha maana ya uraia katika mtazamo wa Kiislamu, na kubainisha maana ya heshima ya nchi na yaliyo wajibu kwa raia.

Kuwahimiza raia kuziba myanya ya chuki na ugomvi na tofauti kati ya jamii moja.

Kuwatahadahrisha raia baadhi ya ufahamu mbaya na kimakosa ambao umesambaa ndani ya baadhi ya jamii za Kiislamu, na ambao unatumiwa katika kuushambulia Uislamu, pamoja na kutoa mafunzo ya kubainisha kati ya ukweli na uzushi, na kuhakikisha usahihi wa habari.

Kumjulisha raia kazi za vyombo vya serikali na wajibu wake katika kusaidia vyombo hivyo, na kumbainishia yaliofanywa na yatakayofanywa na nchi katika wajibu kwenye nyanja mbalimbali ili kuinua nafasi ya nchi na raia[1].

Mwenyezi Mungu Ailinde miji yetu na chuki na uovu, na mkutano wenu huu upate kuwafikishwa na kukubaliwa.

Rehma na amani ziende kwa bwana wetu Muhammad S.A.W. na watu wake pamoja na Masahaba zake.

---

(1) Kitabu cha Yanayohitajika Kulindwa kwenye Neema ya Amani na Utulivu ndani ya Nchi zetu, uk. 121: 124.

Kituo cha Al-Azhar cha Ufasiri

Al-Azhar Al-Sharif ni Taasisi kubwa ya elimu ya Kiislamu ambayo inafanya kazi ya kuhifadhi urithi wa Kiislamu na kuuchunguza kisha kueneza pamoja na kubeba amana ya Ujumbe wa Kiislamu kwa watu wote, inafanya kazi ya kuinua ustaarabu na kusimamia usalama, utulivu na ufariji wa nafsi kwa watu wote duniani na Akhera, kama vile inatoa umuhimu mkubwa wa kueneza ustaarabu wa Kiarabu na urithi wa kielimu na kifikra kwa Umma wa Kiarabu, na kudhihirisha athari ya Waarabu katika ustawi wa ubinadamu na kuendelea kwake, na inafanya kazi pia ya kuinua na kukuza fasihi na maendeleo ya elimu, taaluma huduma za jamii, malengo ya taifa, ubinadamu na misingi ya kiroho, pia kuuongezea ulimwengu wa Kiislamu na wa Kiarabu wasomi wa weledi mbalimbali na wenye fikra kwenye mambo yanayohusu Sharia ya Kiislamu, utamaduni wa Kidini, Kiarabu na lugha ya Qurani.

Kuanzisha Kituo cha Al-Azhar cha Ufasiri:

Katika muktadha wa kuiboresha Al-Azhar Al-Sharif, Mheshimiwa Imamu Mkuu Profesa **Ahmad Al-Tayyib** (Sheikh wa Al-Azhar) ametoa maelekezo ya kuanzisha Kituo cha Ufasiri kinachokusanya vitengo kadhaa vya lugha za kigeni. Kukaanzishwa "**Kituo cha Al-Azhar cha Ufasiri**" kwa maamuzi ya Sheikh wa Al-Azhar namba (49) ya mwaka 2016 A.D. kwa ajili ya kuhudumia sekta zote za Al-Azhar Al-Sharif na kamisheni zake: Ofisi Kuu ya Al-Azhar, Chuo Kikuu, Vikao vya

madarasa, Majopo ya Tafiti za Kiislamu na shule za Al-Azhar katika kila linalohusiana na masuala ya ufasiri unaotegemewa kwenye lugha mbalimbali, **pamoja na kuhakikisha malengo yafuatayo**:

1. Kufasiri vijalada, tafiti na chunguzi mbalimbali ambazo zitahakikisha masilahi ya wote kwa lugha za kigeni zitakazoainishwa na Jopo la Wanazuoni Wakubwa.

2. Kufasiri vijalada na tafiti yakinifu ambazo zinaandikwa ng'ambo kuhusu Uislamu kwa lugha za kigeni.

3. Kufasiri moja kwa moja makongamano na mikutano ambayo inaandaliwa na Al-Azhar Al-Sharif au kamisheni zake.

4. Kuchunguza fasiri za kisasa na za kileo za maana za Qurani Tukufu katika kila lugha, na kuchagua ufasiri ulio bora zaidi na kuyavutia mazingatio ya Waislamu wanufaike nao pamoja na kuueneza ufasiri huo.

5. Kufasiri Hadithi za Mtume S.A.W. kwa lugha mbalimbali, na kuzichunguza fasiri zilizokwishafasiriwa katika uwanja huu, na kuzipitia, pamoja na kuzieneza tena kwa lugha yake na kuyavutia mazingatio ya Waislamu kunufaika nazo.

6. Kufasiri tafiti za fani mbalimbali pamoja na tafiti za kielimu ambazo zinashughulikia masuala ya jamii za Kiislamu zisizokuwa za Kiarabu na masuala yenye utata.

7. Kufasiri hotuba za Ijumaa zinazoshughulikia masuala ya jamii za Kiislamu zisizokuwa za Kiarabu, na kuandaliwa - hotuba hizo - kupitia kamisheni za Al-Azhar Al-Sharif zinazohusika na shughuli hiyo.

8. Kufasiri filamu ambazo zinautambulisha Uislamu kwa umbo la kuvutia na lililoboreshwa na ambalo litaandaliwa na kamisheni za Al-Azhar Al-Sharif zinazohusika na shughuli hiyo.

9. Kutoa kozi katika fani ya ufasiri na uhariri.

10. Kutoa kozi katika fani ya ufasiri wa papo kwa papo.

11. Kutoa jarida thabiti la kielimu linaloelezea Kituo hiki na kazi zake.

12. Kuandaa kozi kwa ajili ya kunyanyua kiwango cha ustadi wa kikazi, kitamaduni, na kielimu kwa wafanyakazi wa Kituo hiki.

Lugha: Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, Kihispania, Kiindonesia, Kiurdu, Kifursi, Kituruki, Kigiriki, Kiposhto, Kiibrania, Kitaliano,

Kiswahili na Kichina. Na hivi sasa kunaundwa timu ya wafanyakazi wa lugha za Kirusi na Kijapani.

Kituo hiki kinawasilisha fasiri zake za mwanzo kwa njia ya mlolongo wa “Ukweli wa Uislamu”. Mlolongo ambao unakusanya vitabu vinavyozitambulisha nyenzo za Uislamu, hadhi ya mtu katika Uislamu na shime ya Uislamu juu ya kuimarisha maadili ambayo yanaitukuza hadhi ya mtu, na kufafanua njia iliyo bora kwa ajili ya kuwatendea vuzuri wanyama, ndege, mimea na vitu vya mada. Kama pia misingi ya Uislamu ilivyoweka wazi kuhusu Muislamu kujilinda ikiwa atashambuliwa au kupigwa vita, ikimlazimisha kujali misingi ya kiutu na kuujenga ulimwengu na siyo kuubomoa. Miongoni mwa vitabu muhimu katika mlolongo huu ni: “Nyenzo za Uislamu” (cha Mheshimiwa Imamu Mkuu Sheikh wa Al-Azhar Prof. **Ahmad Al-Tayyib**, na kitabu cha “Mtu na Maadili katika Dhana ya Kiislamu” (cha Mheshimiwa Prof. **Mahmoud Hamdy Zaqzouq**, Waziri wa Ofisi ya Wakfu ya Misri aliyepita, na kitabu cha “Mtazamo wa Vita katika Uislamu” (cha Sheikh Abu Zahra), na kitabu cha “Mtume wa Uislamu kwa Mtazamo wa fikra ya Kimagharibi” (cha Prof. **Ezz Al Din Faraj**).

Kituo hiki kwa kushirikiana na wasomaji waheshimiwa wanasimamia kila linalohusiana na utoleaji maelezo au maoni, na kusahihisha makosa yoyote ya kilugha au ya kiuchapishaji au makosa mengineyo.

Tunamwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu kwamba fasiri hizi ziwe jiwe jema la msingi katika kuyatakasa maisha ya mtu yatakayoitukuza shani ya watu wote katika kila wakati na pahala, na kuijenga dunia kwa umbo linalowiana na watu.



مشيخة الأزهر

مركز الأزهر للترجمة

Al-Azhar Center for Translation (ACT)